

# Somo la 5: Kuhudumu

*Unaweza kufundisha somo hili kwa ukamilifu wake au kuligawa katika sehemu fupi fupi. Badilisha somo kwa hali ya eneo lako na mahitaji, umri, na uelewa wa urais wako wa akidi au wa darasa..*

## YESU KRISTO ALITUFUNDISHA JINSI YA KUHUDUMU

Ili kuwasaidia washiriki wa urais wa akidi au darasa kumwoka Yesu Kristo kama mfano wao wa kuhudumu, unaweza kuwaalika wazungumze kuhusu mafundisho Yake na mfano wake wa huduma (ona [Luka 10:25–37](#); [3 Nefi 17:5–10](#)). Eleza kwamba kuhudumu ni kumtunza mtu kama vile ambavyo Mwokozi angefanya. Ni lini mtu amefanya hivi kwa ajili yako, na namna gani ilikufanya uhisi? Jinsi gani mfano wa Kristo unatumika kwenye juhudi zetu za kuwahudumia washiriki wa akidi yetu au darasa letu? Kwa wengine?

## TUNAWEZA KUHUDUMU KWA WALE WANAOTUZUNGUKA

Ili kuwasaidia washiriki wa urais wapate msukumo juu ya jinsi ya kuwahudumia washiriki wa akidi au darasa lao, waalike kumjadili kila mtu kwa jina (katibu anaweza kupata orodha ya darasa kutoka kwenye programu ya Zana za Muumini au kwa karani wa kata). Maswali yafuatayo yanaweza kusaidia:

- Tunajua nini kuhusu wao?
- Je! ni upi uwezo wao na changamoto zao za kipekee?
- Je! tunaweza kufanya nini kinachoweza kuwasaidia (kwa mfano, katika huduma na shughuli na mikutano ya Jumapili)?

Waulize washiriki wa urais wazingatie pia ni jinsi gani wanaweza kuwahamasisha washiriki wa akidi au darasa kutumia nguvu na talanta zao kuhudumia wengine, ndani na nje ya akidi au darasa lao.

Alika urais wa akidi au darasa kuchukua hatua juu ya kile wanachohisi kutiwa moyo kufanya. Wanaweza kutaka kufanya marejeo na kurekebisha mipango iliyofanywa katika mkutano wao wa urais wa hivi karibuni ili kuijumuisha mipango yao mipya. Hakikisha wanaelewa kuwa habari nyeti iliyotolewa juu ya watu binafsi inapaswa kutunzwa kama siri.

## NYENZO SAIDIZI

- *General Handbook: Serving in The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints*, [sura ya 21](#), ChurchofJesusChrist.org
- [2 Wakorinto 6:4–7](#); [Mosia 18:8–9](#); [Mafundisho na Maagano 84:106](#)
- ["We Are Strong Together" video](#)